# Afrika yaazimia kuwa sehemu ya suluhisho la mabadiliko ya tabianchi

**NA KHAIRAT HAJI, (ALIYEKUWA NAIROBI).**

VIONGOZI wa Afrika wiki iliyopita walikutana jijini Nairobi, Kenya kwa juma moja kwenye mkutano uliofunguliwa tarehe 4 Septemba 2023 unaohusu Mabadiliko ya Tabianchi.

Mkutano wa kila mwaka ambao unajadili njia mbalimbali za kupunguza utoaji wa gesi chafuzi huku washiriki wakiwa na mbinu za kuweza kukabiliana na athari za tabianchi.

Baada ya majadiliano ya siku tatu, ambayo yamemalizika tarehe 6 Septemba 2023, Afrika imekuja na maazimio yake juu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, pia kutaka mabadiliko ya fedha, na hali ya hewa kutoka katika mataifa ya kaskazini ambayo *yanasemwa kuwa ndio wachafuzi wakubwa wa hali ya hewa*.

Viongozi wa Afrika walijikubalisha kukabiliana na athari za mabadiliko hayo kwa kuyatafutia ufumbuzi ili yasiendelee kuathiri maisha ya wananchi wao.

“Sisi, Viongozi wa Nchi na Serikali za Afrika, tuliokusanyika kwenye mkutano wa Kwanza wa Afrika wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (ACS) hapa Nairobi, Kenya, kuanzia tarehe 4 hadi 6 Septemba 2023, mbele ya viongozi wengine wa dunia, mashirika ya kimataifa, Jumuiya za Uchumi za Kikanda, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, sekta binafsi, mashirika ya kiraia, watu wa asili, jamii za kienyeji, mashirika ya wakulima, watoto, vijana, wanawake, hapa tunatoa maazimio yafuatayo”, lilisema azimio hilo la pamoja.

Katika azimio hilo viongozi wa Afrika walionesha wasiwasi wao kwamba, kwa sasa nchi nyingi za Afrika zinakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo hali ya hewa na mifumo isiyotabirika, ikiwa ni pamoja na ukame wa muda mrefu, mafuriko na moto wa misitu, ambavyo vinazua mgogoro mkubwa wa kibinadamu na athari mbaya kwa uchumi, afya, elimu, amani, na usalama.

**HATUA ZA DHARURA**

Katika hali hiyo viongozi wa Afrika waliitisha hatua za dharura na za pamoja kutoka katika mataifa yote duniani kwa lengo la kupunguza uzalishaji na kupunguza kiasi cha gesi chafu angani ambayo kwa kiasi kikubwa ndio chanzo cha mabadiliko ya tabianchi.

“Tunatambua kwamba Afrika haikuwa na jukumu la kihistoria katika ongezeko la joto duniani, lakini inabeba mzigo wa athari zake, ambao unawaathiri watu, kuanzia afya, maisha, na uchumi wao”, moja ya maelezo kutoka katika azimio.

Viongozi wa Afrika walisisistiza katika azimio hilo kuwa Afrika ina uwezo na azma ya kuwa sehemu ya suluhisho la kimataifa kwa mabadiliko ya tabianchi, kwa kutumia nguvu kazi ya vijana iliyonayo, uwepo wa nishati mbadala, maliasili za kutosha na vitu vyote hivyo vinaweza kutoa suluhisho bora la kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kufikia dhamira zao za kutokuwa na uzalishaji wa kaboni.




*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akihutubia Wakuu wa Nchi mbalimbali, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi Barani Afrika (Africa Climate Summit 23) uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Kenyatta (KICC), Nairobi nchini Kenya wiki iliyopita.*

**JUMUIYA YA KIMATAIFA**

Aidha azimio hilo lilisisitiza juu ya kuitaka jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka katika kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, kutekeleza majukumu yake kama waharibifu wakubwa, kutimiza ahadi za zamani za kulipa fidia, na kusaidia bara la Afrika katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

Kwanza, Kuharakisha juhudi zote za kupunguza uzalishaji ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Mkataba wa Paris, kuheshimu ahadi ya kutoa dola bilioni 100 kila mwaka kama ilivyoahidiwa miaka 14 iliyopita katika mkutano wa Copenhagen.

Sambamba na hilo, lakini viongoai hao walitaka kutekelezwa ahadi za kusitisha kwa haraka matumizi ya makaa ya mawe na kufuta ruzuku zote za nishati zenye sumu.

Pia azimio linaitisha uwekezaji chanya kwenye masuala ya hali ya hewa ambayo yataleta mwelekeo wa ukuaji wa uchumi na kubadilisha sayari ya dunia na kuwezesha nchi za Afrika kufikia hadhi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2050.

Katika azimio hilo viongozi wa Afrika wameahidi kuendeleza na kutekeleza sera na kanuni zinazolenga kuwavutia wawekezaji wa ndani, wa kikanda na wa kimataifa katika ukuaji wa kijani na uchumi wenye uwiano, ili kuweza kukidhi haja ya kukabiliana na athari kama ukame, mafuriko na nyenginezo.

**USALAMA WA CHAKULA**

Kuhusu usalama wa chakula mkutano huo umeone kuwa ni moja ya eneo muhimu la kuzungumziwa hasa athari za mabadiliko ya tabianchi, na katika azimio hilo la Nairobi.

Viongozi wa Afrika wamekubaliana kuimarisha juhudi katika kuongeza mavuno ya kilimo na kuondokana na kulima kwa mazoea ambapo hakutoi usalama na uhakika wa mavuno.

Aidha Afrika ikibadilisha utamaduni wa kulima kimazoea, itaboresha zaidi usalama wa chakula hasa katika kipindi ambacho watakumbwa na athari mbaya za mazingira.

Azimio pia liliweka mkazo katika kuunga mkono wakulima wadogo na jamii za kienyeji kwa kuwasikiliza, kuwashirikisha na kuwasaidia inapobidi, kwa kuwa na wao wana jukumu na nafasi muhimu katika utunzaji wa mazingira ya teknolojia.

“Tunasisitiza umuhimu wa kukubali maarifa ya watu wa asili na sayansi ya raia katika mikakati ya uboreshaji na mifumo ya tahadhari mapema”, lilisema azimio.


Aidha, viongozi wa Afrika wanaitisha ushirikiano wenye ufanisi kati ya nchi zote Afrika na maeneo mengine, ili kukidhi mahitaji ya msaada wa kifedha, kiufundi na kiteknolojia, na kusaidiana maarifa kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujikinga na athari zake.

Jambo la muhimu pia katika kujikinga na athari za mabadiliko hayo, Afrika imeamua kuimarisha mifumo ya tahadhari mapema kupitia habari za hali ya hewa, pamoja na kuchukua hatua za haraka za kulinda maisha ya watu wake na mali zao.

Hayo ni baadhi ya maazimio kutoka katika mkutano huu mkubwa na wa kwanza kufanyika barani Afrika, ambao umehudhuriwa na marais 15 kutoka nchi za Afrika pamoja na viongozi mbali mbali wa jumuiya za kitaifa, kikanda na kimataifa.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulijadili namna ya kupata suluhisho za athari za mabadiliko ya tabianchi, ambayo ni matumaini ya kila muafrika.

Hivyo, azimio hilo likifanyiwa kazi ipasavyo litasaidia sana kupunguza athari zinazoikumba Afrika kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.



*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye picha ya pamoja na Wakuu wa Nchi mbalimbali za Afrika, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi Barani Afrika (Africa Climate Summit 23) Nairobi nchini Kenya wiki iliyopita.–*